



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

Kumb. Na. HWB/L. 20/26/7

15 Februari, 2022

Kuh: **TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA
ANUANI YA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo anapanda kuwatangazia nafasi za Ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la Anwani za makazi katika Kata, Vijiji na Mitaa ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

A. SIFA ZA MWOMBAJI: -

- i. Awe Raia wa Tanzania mwenye Umri wa miaka 18 – 35
- ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea
- iii. Awe anamiliki simu janja *Android* yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima
- iv. Awe na barua pepe (email) na nywila (Password) inayofanya kazi
- v. Awe na uwezo wa kusoma ramani za Vijiji/Mitaa

B. KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- iii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa Anuani ya Makazi.
- iv. Kutuma *Data* kwenye mfumo wa Anuani ya Makazi

C. MAOMBI YAAMBATISHWE NA: -

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
- ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- iii. Picha (Passport size 2)
- iv. Barua ya maombi ipite kwa Afisa Mtendaji wa Kata aliyepo mwombaji
- v. Hakikisha unaandika namba zako za simu ya mkononi kwenye barua yako

N.TEHAMA

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, S.L.P 59 BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.
Simu Na: 023 2440164, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz. Tovuti: www.bagamoyo.go.tz

D. MALIPO

Malipo yatafanyika kwa kiasi cha kazi kwa siku.


E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

i. Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anuani kamili ya mwombaji, namba za simu, barua pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kupitia kwa Mwenyekiti wa Kitongoji na Mtendaji wa Kata husika.

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo,
S. L. P 59,
BAGAMOYO.

F. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 22/02/2022 (Jumanne) Saa 9:30 Alasiri.

Limetolewa na:-


Shauri Selejda
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO.

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
BAGAMOYO**

WTEHAMA

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, S.L.P 59 BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.
Simu Na: 023 2440164, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz. Tovuti: www.bagamoyo.go.tz